## Idara ya Vermont ya Watoto na Familia (DCF) ni shirika la serikali linalohusika na kulinda watoto na kuimarisha familia.

Kitengo chetu cha Huduma za Familia (FSD) kinashirikiana na familia na wengine kusaidia kuhakikisha watoto na vijana:

- Wako salama kutokana na unyanyasaji
- Wametimiziwa mahitaji yao ya kimsingi (mfano, chakula, mavazi, makazi, na huduma za afya)
- Wanapata utunzaji, usaidizi, na usimamizi wa wazazi wanaohitaji ili kuhakikisha ustawi wao na elimu

## Kwa nini FSD iliwasiliana na familia yangu?

Kuna uwezekano mkubwa kwamba tulipigiwa simu na mtu ambaye alikuwa na wasiwasi kuhusu usalama na ustawi wa mtoto wako.

Simu hiyo inaweza kuwa imetoka kwa mtu wa familia, rafiki, jirani, au mtu mwingine anayemjua mtoto wako.

Mtu yeyote anaweza kupiga simu ili kutoa wasiwasi wao juu ya mtoto. Watu wengine, kama madaktari, walimu, na watoa huduma ya utunzaji wa watoto, wanatakiwa kisheria kuripoti unyanyasaji au utelekezwaji wowote wa watoto.

**Hizi simu zinajulikana kama *ripoti.***

## Ripoti mliyopokea kuhusu familia yangu ilishughulikiwa kivipi?

### Msimamizi:

1. Alipitia ripoti hiyo.
2. Alizingatia mambo kama vile umri wa mtoto wako na asili ya wasiwasi uliowasilishwa.
3. Aliamua kuwa msaada (uingiliaji) ulihitajika – kulingana na sheria ya Vermont na sera ya FSD.
4. Alichagua uingiliaji mwafaka: tathmini au uchunguzi.
   *Katika visa vingine, sheria inatutaka tufanye uchunguzi. Hii ni pamoja na wakati wowote kuna tuhuma kwamba mtoto alidhalilishwa kingono na mtu mzima.*
5. Alikabidhi kesi yako kwa mfanyakazi.
   *Uingiliaji uliochaguliwa kawaida huanza ndani ya masaa 72. Inawezekana huo ndio wakati utakapojulishwa kwamba tunahusika katika familia yako.*

Mfanyakazi hawezi kukufichulia utambulisho wa mtu aliyetoa ripoti. Utambulisho wake unaweza kufichuliwa ikiwa ripoti hiyo itasababisha mashtaka ya mahakama au ya bodi ya huduma za kibinadamu.

## Uingiliaji kati unaanzaje?

### Katika uchunguzi:

1. Mfanyakazi atamhoji au kumchunguza mtoto katika ripoti hiyo.
   *Sheria inaturuhusu kufanya hivi bila ufahamu au ruhusa yako ikiwa imethibitishwa.*
2. Mtu asiyeegemea upande wowote kama vile mwalimu au muuguzi wa shule atakuwepo wakati wa mahojiano.
3. Tutakuambia kuhusu mahojiano na kuripoti haraka iwezekanavyo baadaye.

### Katika tathmini:

1. Mfanyakazi atawasiliana nawe kujadili wasiwasi ulioripotiwa.
2. Anaweza kuomba ruhusa yako kuzungumza na au kumchunguza mtoto katika ripoti.
3. Ukikataa, bado tunaweza kuamua kufanya uchunguzi ikiwa kuna wasiwasi wa usalama.

**Tunahitaji kuendelea kuwasiliana!**
Hakikisha kutujulisha:

- Njia bora ya kuwasiliana na wewe (kwa mfano, anwani ya barua pepe).
- Ikiwa hali yako ya makazi au anwani ya barua pepe inabadilika.

## Ni nini hufanyika wakati wa kuingilia kati?

Hatua zifuatazo zinaweza kutokea kwa uchunguzi na tathmini.

### Hatua ya 1: Kutathmini usalama wa mtoto

Mfanyakazi atatumia *Zana ya Tathmini ya Usalama ya SDM®* ili:

a. Kutathmini usalama wa haraka wa mtoto wako.
b. Ataamua ikiwa mtoto wako ni *salama*, *salama na mpango*, au *si salama*.

### Hatua ya 2: Kutathmini hatari ya familia

Mfanyakazi atatumia *Zana ya Tathmini ya Hatari ya SDM®* ili:

a. Kutathmini hatari ya madhara ya baadaye bila kuingilia kati.
b. Kuamua kiwango cha hatari: *chini*, *wastani*, *juu*, au *juu sana*.

### Hatua ya 3: Kuamua matokeo

Ikiwa hatari ni *kubwa* au *kubwa sana*, tunaweza kufungua kesi kwa huduma zinazoendelea ambazo zitasaidia kufanya familia yako kuwa thabiti.

Ikiwa tulifanya uchunguzi, tutabaini ikiwa unyanyasaji au utelekezaji ulioripotiwa ulitokea. Kama NDIVYO:

- Madai ya ripoti hiyo yatathibitishwa.
- Jina la mtu aliyethibitishwa linaweza kuongezwa kwenye Sajili ya Ulinzi wa Watoto.

## Ni nini kinachotokea baadaye?

Ikiwa tumefungua kesi ya huduma zinazoendelea, tutakusaidia kuendeleza mpango wa kufanya nyumba yako kuwa salama, kumweka mtoto wako nyumbani na kuimarisha familia yako.

Hii ni pamoja na:

1. Kutathmini hali ya mtoto wako (kwa mfano, afya ya mwili na akili).
2. Kutambua uwezo na changamoto za familia yako. Hii ni pamoja na masuala unayohitaji kushughulikia na kile kinachoyasababisha.
3. Kujenga mtandao wa familia na marafiki ambao wanaweza kusaidia.
4. Kutambua huduma na misaada ambayo itasaidia familia yako. Hii inaweza kujumuisha, kwa mfano, ushauri nasaha, madarasa ya malezi, mafunzo ya kazi, na matibabu ya uraibu wa dawa za kulevya na kupata nafuu.

## Je, mtachukua mtoto wangu?

Jibu kwa kawaida huwa LA.

Ikiwa tunaamini mtoto wako sio salama hata hivyo, tunaweza kuiomba mahakama kuangalia tena hali hiyo. Kisha jaji atatoa uamuzi.

## Ninaweza kupata wapi maelezo zaidi?

Tembelea dcf.vermont.gov/fsd ili:

- ➲ Kujifunza kuhusu sheria, sera na kanuni zinazoongoza kazi yetu kwa watoto, vijana na familia.
- ➲ Kupata nakala ya *Mwongozo wa Mzazi kwa Kitengo cha Huduma za Familia cha DCF*.
- ➲ Kupata nakala za machapisho mengine.

## Ninaweza kupata wapi msaada wa ziada?

Mfanyakazi wako anaweza kukuunganisha na mipango ambayo inaweza kusaidia familia yako.

Unaweza pia kupata msaada peke yako. Mahali pazuri pa kuanzia ni kwenye tovuti ya DCF. Nenda kwenye dcf.vermont.gov kupata mipango ambayo inaweza kukusaidia:

- ➲ Kutimiza mahitaji ya msingi ya familia yako (kwa mfano, utunzaji wa watoto, nishati, chakula, mafuta na maji).
- ➲ Kuhakikisha ukuaji na ustawi wa afya ya watoto wako.
- ➲ Kufikia malengo ambayo yatakusaidia kutunza familia yako kifedha.

Unaweza pia kupata maelezo kuhusu nyenzo nyingine zinazopatikana kwa kupiga 2-1-1 kutoka mahali popote katika Vermont.

## OFISI ZA WILAYA

Barre: (802) 479-4260

Bennington: (802) 442-8138

Brattleboro: (802) 257-2888

Burlington: (802) 863-7370

Hartford: (802) 295-8840

Middlebury: (802) 388-4660

Morrisville: (802) 888-4576

Newport: (802) 334-6723

Rutland: (802) 786-5817

Springfield: (802) 289-0648


St. Albans: (802) 527-7741

St. Johnsbury: (802) 748-8374

**MJULISHE MHUDUMU WAKO:**

- **Lugha unayoweza kuzungumza na kusoma kwa urahisi zaidi.**
- **Ikiwa ungependa huduma za tafsiri za bila malipo ili kuhakikisha kuwa unaelewa mawasiliano yetu.**
- **Ikiwa unahitaji marekebisho adilifu kwa sababu wewe au mtoto wako ana ulemavu.**

10,000 • 07/22






*Mwongozo wa Mzazi kwa*

# Hatua za Usalama wa Mtoto

VERMONT

DEPARTMENT FOR CHILDREN & FAMILIES

FAMILY SERVICES DIVISION